BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

KIDATO CHA NNE

015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

(Kwa Watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

MUDA: Saa 3 **Jumatatu, 31 Agosti 2026 Mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili (2) kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16),** sehemu B ina alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30)**.
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Shulelibrary.com

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

   (i) Sara baada ya kuhitimu elimu yake ya Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro alionekana kusimamisha swala tano na kuvaa stara muda wote tofauti na alivyokuwa mwanzoni. Hali hii inaashiria nini kwa Sara?
   - A. Inaonesha kuwa Sara ni muoga wa sheria za Chuo
   - B. Inaonesha kuwa ameelimika
   - C. Inaonesha kuwa Sara amekua
   - D. Inaonesha kuwa a Sara ni Muislamu safi
   - E. Inaonesha kuwa Sara ni mwanamke bora

   (ii) MV Bukoba wakati inazama katika ziwa Viktoria kuna kafiri mmoja alisikika akimuomba Mwenyezi Mungu kwa dhati kabisa ili awaokoe. Ni kitu gani kilichompa msukumo huo wakati yeye alikuwa hakubali uwepo wa Mwenyezi Mungu?
   - A. Woga wa kifo
   - B. Kufuata mkumbo
   - C. Alisilimu ghafla
   - D. Fitra aliyopandikizwa
   - E. Alishauriwa afanye hivyo

   (iii) Moa ni kijana ambaye amejitenga na jamii kwa ajili ya kufanya ibada na amesema hataoa na muda mwingi atafunga na angetengana na mambo ya maendeleo ya dunia ili apate pepo. Kwa mujibu wa mtazamo wa Uislamu juu ya dini, yeye tunamuweka katika kundi gani?
   - A. Wapagani
   - B. Makafiri
   - C. Washirikina
   - D. Watawa
   - E. Wacha Mungu

   (iv) Ukiwa kama mwanafunzi uliyeelimika kutoka Madrasatul Ahbaab, waelimishe wanajamii yako juu ya mtazamo wa Uislamu kuhusu Fiqh.
   - A. Ni elimu ya Kiislamu inayohusiana na mambo ya sharia
   - B. Ni elimu ya Kiislamu inayohusiana na kumfuata Allah (S.W)
   - C. Ni elimu ya Kiislamu inayohusiana na kumpwekesha Allah (S.W)
   - D. Ni elimu ya Kiislamu inayohusiana na ufafanuzi wa nguzo za Imani

   (v) Abdallah aliulizwa swali na kafiri mmoja kuwa iwapo Mwenyezi Mungu (S.W) ameumba, yeye kaumbwa na nani? Abdallah alipaswa kumsomea sura gani ili kujibu swali lake?
   - A. Suratul Fat-ha
   - B. Suratul Nasir
   - C. Suratul Kaafirun
   - D. Suratul Mau'un
   - E. Suratul Ikhlas

Shulelibrary.com

(vi) Mwenyezi Mungu (S.W) alimuandaa Mtume Muhammad (S.A.W) kuwa kiongozi mahiri ambaye hapakuwa na mfano wake. Kutokana na maandalizi hayo tunafundishwa sifa gani ya kiongozi?

A. Mwenye kusimamisha haki na kuchukia maovu
B. Mwenye kufanya biashara kwa uadilifu
C. Mwenye kuwa na elimu dunia na akhera
D. Mwenye kupenda makabila na kusifiwa kwa tabia
E. Mwenye kupenda vijana tu wanaohitaji msaada

(vii) Adam (A.S) na mkewe walimkosea Mwenyezi Mungu (S.W) na Ibilisi pia alimkosea Mwenyezi Mungu (S.W). Ni ipi tofauti ya msingi ya wakosaji hawa?

A. Ibilisi alikula tunda lakini Adam na mkewe walishawishiwa na Ibilisi
B. Adam na mkewe waliadhibiwa na kuletwa duniani lakini Ibilisi alibaki peponi
C. Adam na mkewe walitubia lakini Ibilisi alileta kibri akalaaniwa
D. Kosa la Adam na mkewe lilikuwa zito lakini kosa la Ibilisi halikuwa zito
E. Kosa la Adam na mkewe ni la kibinadamu lakini kosa la Ibilisi ni la kijini

(viii) Joel alitamka shahada mbili aliposilimu. Ipi ni miongoni mwa tabia atakazozionesha kuthibitisha anaifanyia kazi sehemu ya kwanza?

A. Hataacha kutekeleza aliyofundisha Mtume (S.A.W)
B. Atamtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake
C. Hataacha kuwaombea dua maswahaba
D. Atatekeleza nguzo zote za Uislamu
E. Hatamshirikisha Mwenyezi Mungu (S.W)

(ix) Bwana Kabo alipokuwa anapigana vita ya kisheria vya Kiislamu alifariki. Ni mambo yapi hakufanyiwa katika mambo anayofanyiwa maiti wa Kiislamu?

A. Kuswaliwa na kuzikwa
B. Kuoshwa na kuzikwa
C. Kukafiniwa na kuzikwa
D. Kuoshwa na kukafiniwa
E. Kuzikwa na kuombewa dua

(x) Uandishi wa Hadith za Mtume (S.A.W) umepitia vipindi kadhaa. Ni kipindi gani ambacho wanazuoni wa fani hiyo walifanikiwa kuandika vitabu sita vinavyotegemewa?

A. Kipindi cha Tabiin
B. Kipindi cha Mtume (S.A.W)
C. Kipindi cha Tabii Tabiin
D. Kipindi cha Makhalifa
E. Kipindi cha Maswahaba

shuleilibrary.com

2. Oanisha maelezo ya matendo yanayokamilisha ibada ya Hijja yaliyopo katika orodha A na matendo husika ya ibada hiyo yaliyopo katika orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia mbele ya namba ya Kirumi.

ORODHA A		ORODHA B
(i)	Kuzunguka al-Kaaba ambako bila ya kufanya hivyo ibada ya Hijjah haiswihi	A. Talbiya B. Widaa
(ii)	Baada ya tendo hilo Hajji anayefanya Umrah tu hunyoa nywele na kuvua ihram	C. Ihram D. Tawaful Ifadha
(iii)	Hajji (mwanaume) hufanya "Iztibaa" wakati wa kutekeleza mzunguko huo	E. Kusimama Arafa F. Tawaful Qudum
(iv)	Maneno anayosema Hujaji kuashiria kuanza kwa ibada ya Hijjah au Umrah	G. Sa'i H. Kulala Muzdalifah
(v)	Ni sunnah kunyoa nywele, kuoga na kupaka manukato kabla ya kuvaa vazi hilo	
(vi)	Ni kitendo cha nguzo ya Hijjah kinachohusisha Hujaji kuwepo sehemu fulani mwezi 9 Dhulhijjah	

SEHEMU B (Alama54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. Tumepewa amri ya kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu (S.W) kama msingi mmojawapo wa Imani ya Kiislamu. Kwa kutumia hoja sita (6), onesha faida atakazozipata mtu atakayekuwa na Imani thabiti juu ya nguzo hiyo.

4. Katika jamii kuna kampeni nyingi za kudhibiti uzazi, ambazo hazina faida bali ni hasara tu. Kwa mujibu wa Uislamu, bainisha madhara matatu ya kufuata kampeni hizo.

5. Pamoja na mazingira magumu yaliyopo ya utekelezaji wa haki na uadilifu katika jamii, bado hatupaswi kukata tamaa katika kuyaishi maisha hayo. Fafanua mambo matatu ambayo jamii ikiyazingatia watapata wepesi wa kuyaishi maisha hayo.

6. Misikiti yetu imebakia kuwa sehemu kwa ajili ya swala tano tu, kisha watu hutawanyika tofauti na ilivyokuwa wakati wa Mtume (S.A.W). Kwa kuzingatia ujuzi wako wa historia ya Uislamu, tumia dondoo sita (6) kuelimisha jamii yetu juu ya matumizi mengine ya taasisi hiyo.

7. Ili dhana ya makosa katika sheria ya Kiislamu ieleweke vizuri, imewekwa katika nyanja tatu. Bainisha Nyanja hizo kwa kutoa mfano katika kila nyanja.

8. Umar bin Abdul-Aziz ni kiongozi wa Kiislamu ambaye baadhi ya wanachuoni wa Kiislamu wamempa hadhi kama Khalifa wa tano wa Dola ya Kiislamu. Eleza kwa ufupi mambo sita (6) yaliyosababisha apewe hadhi hiyo.

Shulelibrary.com

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** katika sehemu hii

9. Utafiti uliofanyika unaonesha kuwa Waislamu wengi wanakwenda kufanya ibada ya Hijjah lakini wakisharejea baadhi yao hawaonekani wakiathiriwa na ibada hiyo. Kwa kutumia dondoo nne (4) eleza nini kifanyike ili waweze kupata athari njema za ibada hiyo.

10. Matini ya Hadith ni maneno ya Mtume (S.A.W) au maneno ya Maswahaba wake kuhusu yale aliyoyafanya. Chambua masharti yake matano (5) ili iwe sahihi.

11. Jomo alichanganywa na kauli ya muhubiri mmoja wa Injili aliyedai kuwa Qur'an ni zao la shetani na hakuwa na elimu kumpinga. Je, ungekuwa wewe ungetumia hoja zipi kumpinga muhubiri huyo? Toa hoja nne (4).

Wabillah Tawfiiq

Shulelibrary.com